FUNZO LA 50

1. Kwa nini Shetani alimjaribu Yesu?
-Kwa sababu Shetani alitaka Yesu atende dhambi.

2. Kwa nini Shetani alitaka Yesu atende dhambi?
-Kwa sababu Shetani hakutaka Yesu atuokoe.

3. Je, Yesu angeweza kugeuza mawe kuwa mkate?
-Ndiyo.
-Yesu alikuwa Mungu.
-Yesu angeweza kufanya chochote.

4. Ni nini Yesu alimwambia Shetani ni muhimu kuliko chakula?
-Yesu alimwambia Shetani kuwa kuliamini Neno la Mungu ni muhimu kuliko chakula.

5. Ijapokuwa Yesu alikuwa na njaa, kwa nini hakugeuza mawe kuwa mkate?
-Kwa sababu Mungu Baba hakumwambia afanye hivyo.
-Yesu hangemtii Shetani.
-Yesu angemtii tu Mungu Baba.

6. Je, Shetani anajua yaliyoandikwa katika Biblia ya Mungu?
-Ndiyo.

7. Lakini Shetani hufanya nini na Neno la Mungu?
-Shetani analingeuza Neno la Mungu ili kuwanasa watu.



8. Kwa nini iliwezekana kwa Shetani kumpa Yesu udhibiti wa ulimwengu wote?
-Kwa sababu wakati Adamu alimtii Shetani, Shetani alikuwa bwana wa Adamu, wa watu wote, na wa ulimwengu wote.

9. Je, Yesu alimshindaje Shetani?
-Kwa Neno la Mungu.

10. Je, Yesu alilingeuza Neno la Mungu?
-La.
-Yesu alizungumza Neno la Mungu kama ilivyoandikwa katika Biblia ya Mungu.

11. Ni nani aliye mkuu, Yesu au Shetani?
-Yesu.

12. Kwa nini Yesu ni mkuu kuliko Shetani?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.
-Kwa sababu ni Yesu aliyemuumba Lusifa kama malaika mkamilifu hapo mwanzo.

13. Katika siku zijazo, je, Yesu atamfanya nini Shetani na mapepo wake wote?
-Yesu atamtupa Shetani na mapepo wake wote katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Siku moja, Mfalme mwovu Herode alimweka Yohana Mbatizaji gerezani.
-Baada ya Yohana Mbatizaji kuwekwa gerezani, je Yesu alifanya nini?

Tusome Marko 1:14

14-Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri habari njema ya Mungu,.

-Je, Yesu alianza kufundisha Wayahudi lini?
-Baada ya Yohana Mbatizaji kuwekwa gerezani.

-Yesu alikuwa na umri gani wakati alianza kufundisha Wayahudi?
-Alikuwa na umri wa miaka 30.

-Yesu aliwafundisha Wayahudi Habari Njema ya Mungu.

-Ni Nini Habari Njema ya Mungu ambayo Yesu alifundisha?

-Habari Njema ya Mungu ni kwamba ingawa dhambi zetu lazima ziadhibiwe na kifo, Mungu alikuwa anamtuma Mwokozi kutuokoa.

-Mwokozi ambaye Mungu alikuwa anamtuma kuokoa watu ni nani?
-Yesu.

-Ni nini kingine Yesu alifundisha?

Tusome Marko 1:15

15-Akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.



-Yesu alimaanisha nini aliposema, "Wakati umefika, na ufalme wa Mungu umekaribia"?

-Yesu alimaanisha kwamba wakati umefika wa Mwokozi, na kwamba ufalme wa Mungu utashinda ufalme wa Shetani hivi karibuni.

-Yesu pia alifundisha kwamba watu lazima waamini Neno la Mungu.

-Ni njia gani pekee ambayo mtu anaweza kumpendeza Mungu?
-Kwa kuamini Neno la Mungu.

-Yesu alipoanza kuwafundisha Wayahudi, aliwaita watu wawe pamoja naye.

Tusome Marko 1:16-20

16-Naye alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya, akamwona Simoni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi.
17-Yesu akawaambia, Njoni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.
18-Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata.
19-Akaendelea mbele kidogo, akamwona Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, nao pia walikuwa chomboni, wakizitengeneza nyavu zao.
20-Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya chombo pamoja na watu wa mshahara, wakaenda, wakamfuata.

-Kwa nini Yesu aliwaita watu kuwa pamoja naye?

-Kwa sababu Yesu alitaka kuwafundisha ili waweze kuwafundisha watu wengine juu ya Mungu.

-Ni kazi gani baadhi ya watu aliowaita Yesu kuwa naye walifanya?
-Baadhi yao walikuwa wavuvi.

-Siku moja, Yesu alikwenda mji uitwao Kapernaumu kuwafundisha Wayahudi.

Tusome Marko 1:21

21-Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi, akafundisha.

-Yesu alipofika Kapernaumu, alienda kwenye sinagogi kufundisha.

-Sinagogi ilikuwa nini?

-Sinagogi ilikuwa nyumba ambayo Wayahudi walikutana kusoma Biblia.

-Wayahudi wengi walifikiria nini juu ya mafundisho ya Yesu?

Tusome Marko 1:22

22-Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana



alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi.

-Kwa nini Wayahudi wengi walishangazwa na mafundisho ya Yesu?
-Kwa sababu Yesu aliwafundisha kwa nguvu nyingi na hekima.

-Walimu wa sheria walikuwa nani?
-Walikuwa Mafarisayo.

-Ni jinsi gani mafundisho ya Yesu yalikuwa tofauti na mafundisho ya Mafarisayo?

-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu alimjua Mungu Baba.
-Mafarisayo hawakumjua Mungu Baba.

-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu alijua Neno la Mungu.
-Mafarisayo hawakujua Neno la Mungu.

-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu, Yesu aliamini Neno la Mungu.
-Mafarisayo hawakuamini Neno la Mungu.

-Yesu alipokuwa akifundisha, mtu mmoja aliyekuwa na pepo alilia.

Tusome Marko 1:23-24

23-Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu

mwenye pepo mchafu; akapaza sauti,

24-akisema, Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuangamiza?

-Hapo mwanzo, mapepo walikuwa nani kabla ya kuwa mapepo?

-Mwanzoni, mapepo walikuwa malaika wazuri ambao Mungu aliwaumba hadi walipomfuata Shetani na kuwa wabaya.

-Mapepo hupenda kuishi katika watu wasiomwamini Mungu.

-Pepo alikuwa akiishi ndani ya mtu huyu ambaye alilia.

-Je pepo alijua kuwa ni Yesu aliyekuwa akifundisha?
-Ndiyo.
-Je, mapepo wanajua kuwa Yesu ni Mungu?
-Ndiyo.

-Je, mapepo wanajua kwamba Yesu ni mkamilifu, mtakatifu, na anachukia dhambi zote?
-Ndiyo.

-Je, pepo wanajua kuwa Yesu ana nguvu kuliko wao?
-Ndiyo.

-Kwa nini mapepo yanamwogopa Yesu?

-Kwa sababu mapepo wanajua kwamba Yesu anaweza kuwatupa katika Ziwa la Moto wa Milele wakati wowote.



-Pepo huyo alijua kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kumtupa katika Ziwa la Moto wa Milele wakati huo.

-Yesu alimjibu nini yule pepo?

Tusome Marko 1:25-26

25-Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke.

26-Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka.

-Yesu alimwamuru yule pepo anyamaze, na kutoka kwa yule mtu.

-Je, huyo pepo alimtii Yesu?
-Ndiyo.
-Kwa nini pepo alimtii Yesu?

-Kwa sababu Yesu ni Mungu.
-Kwa sababu Yesu ana nguvu kuliko pepo.

-Watu walifikiria nini walipomwona Yesu akimuokoa yule mtu kutoka kwa yule pepo?

Tusome Marko 1:27-28

27-Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema, Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii!

28-Habari zake zikaenea mara kotekote katika nchi zote kandokando ya Galilaya..

-Watu walishangaa kwamba Yesu alimwokoa yule mtu kutoka kwa yule pepo.

-Watu walishangaa kwamba pepo walimtii Yesu.

-Baadaye jioni hiyo, nini kilitokea?

Tusome Marko 1:32-34

32-Hata kulipokuwa jioni, na jua limekwisha kuchwa, walikuwa wakimletea wote waliokuwa hawawezi, na wenye pepo.
33-Na mji wote ulikuwa umekusanyika mlangoni.
34-Akaponya wengi waliokuwa na maradhi mbalimbali, akatoa pepo wengi, wala hakuwaacha pepo kunena, kwa sababu walimjua.

-Jioni hiyo, watu walimletea Yesu wagonjwa wote na wenye pepo, na Yesu akawaponya wote.

-Hii ni kwa sababu Yesu ni Mungu.
-Hii ni kwa sababu Yesu anaweza kufanya chochote.

-Kwa nini Yesu aliwaponya wagonjwa wote?

-Kwa sababu Yesu aliwapenda.
-Kwa sababu Yesu alikuwa na huzuni kwamba walikuwa



wagonjwa.

-Mwanzoni wakati Yesu aliumba ulimwengu, hakukuwa na ugonjwa.

-Lakini Adamu na Hawa walimkosea Mungu, na dhambi yao ilileta magonjwa kwa watu wote.

-Yesu alitaka kuponya magonjwa ambayo dhambi imeleta ulimwenguni.

-Kwa nini Yesu aliwaponya watu wote waliokuwa na pepo?
-Kwa sababu Yesu aliwapenda.

-Kwa sababu Yesu alikuwa na huzuni kwamba mapepo yalikuwa yanawafanya watu kuwa watumwa wao.

-Mwanzoni wakati Yesu aliumba ulimwengu, watu walikuwa watoto wa Mungu.

-Lakini Adamu na Hawa walimkosea Mungu, na watu wote wakawa watumwa wa Shetani na mashetani wake.

-Yesu alitaka kuwakomboa watu kutoka katika utumwa wa Shetani na mashetani wake.

-Siku moja mtu mwenye ukoma alikuja kumwona Yesu.

Tusome Marko 1:40

40-Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, Ukitaka, waweza kunitakasa.

-Ukoma ni nini?
-Ukoma ni ugonjwa mbaya sana ambao unakula mwili wako.

-Katika wakati wa Yesu, hakukuwa na tiba ya ukoma.

-Kama ulikuwa na ukoma, hakukuwa na dawa kwako.
-Kama ulikuwa na ukoma, hakukuwa na tiba kwako.
-Kama ulikuwa na ukoma, hakukuwa na msaada kwako.

-Je, Mtu huyo aliweza kujiponya na ukoma?
-La.
-Hakukuwa na tiba.

-Je, kulikuwepo na mtu mwingine aliyeweza kumponya kutokana na ukoma?
-La.
-Hakukuwa na tiba.

-Daktari aliweza kumponya ukoma?
-La.
-Hakukuwa na tiba.

-Kwa nini mtu huyo alikuja kwa Yesu?
-Kwa sababu alijua kuwa Yesu peke yake ndiye aliyeweza kumponya.

-Yesu alimponya?





41-Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika.
42-Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika.

-Yesu alimgusa yule mtu, akasema, “Takasika,” na mtu huyo akapona.

-Ni Yesu tu ambaye ni Mungu ndiye aliyeweza kumponya huyo mtu.
-Ni jinsi gani dhambi inafanana na ukoma?

-Kama vile mtu huyo hakuweza kujiponya na ukoma, kwa hivyo sisi hatuwezi kujiponya wenyewe kutoka kwa dhambi.

-Kama vile hakuna mtu mwingine aliyeweza kumponya mtu huyo kutoka kwa ukoma, kwa hivyo hakuna mtu mwingine anayeweza kutuponya sisi kutoka kwa dhambi.

-Kama vile Yesu tu ndiye aliyeweza kumponya mtu huyo kutoka kwa ukoma, ndivyo tu Yesu ndiye anayeweza kutuponya sisi kutoka kwa dhambi.

-Yesu alikuja ulimwenguni kutuponya dhambi.
-Yesu alikuja ulimwenguni kutuponya kutoka kwa kifo.
-Yesu alikuja ulimwenguni kutuponya kutoka kwa Shetani.

-Hakuna mtu mwingine anayeweza kutuponya; ni Yesu tu anayeweza kutuponya.